



Anansi na Sungura walikuwa marafiki.

Anansi alionea wivu mali ya Sungura.



Anansi alimfukuza
Sungura.

Akachukuwa shamba
lake.



Anansi aliuza mazao
yote.

Alipata pesa nyingi.



Anansi alirudi
nyumbani.

Alikibeba kikapu
kichwani.



Anansi alikiweka
kikapu chini.

Alienda kujikinga
asinyeshewe.



Muvua ilisababisha
mafuriko.

Anansi alijificha
shimoni.



Tai alikiona kikapu.

Alikifunika kwa
mabawa yake.



"Kikapu hiki ni changu," Tai alisema.

"Ni changu!" Anansi alipiga kelele.




Tai alisema, "Nilipata mahindi na pesa bila mwenyewe."



Chifu na wazee wake walichukuwa muda kuamua nani alisema ukweli.



Hatimaye, walisema,
"Tai anasema ukweli.
Kikapu ni chake."



Sungura alirudi katika shamba lake.

Anansi hakuwa na pesa wala marafiki.